MAJI TANZANIA

TOLEO NA 022

OKTOBA- DESEMBA, 2023

# Miradi ya maji mfano wa kuigwa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameipongeza Wizara ya Maji kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maji.

Wizara ya Maji. inayoongozwa na Mhe. Jumaa Aweso (Mb) imepewa pongezi pamoja na Wataalamu wa Wizara hiyo kwa matumizi mazuri ya fedha za miradi katika utekelezaji na usimamizi mzuri nchini,na kuagiza iwe mfano katika miradi mingine yote ya serikali.






# Makamu wa Rais asisitiza ulinzi wa mazingira, pamoja na vyanzo vya maji

## Mradi wa Maji wa Miji 28 Kukamilika kwa Wakati – Aweso

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amehawahakikishia Watanzania kuwa mradi wa maji wa miji 28 utakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa mwaka 2025.
Mhe. Aweso amesema hayo akiwa jijini New Delhi nchini India alipofanya mazungumzo na viongozi wa makampuni ya wakandarasi wanaotekeleza mradi huo .



# Miradi ya maji mfano wa kuigwa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameipongeza Wizara ya Maji kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maji.
Wizara ya Maji. inayoongozwa na Mhe. Jumaa Aweso (Mb) imepewa pongezi pamoja na Wataalamu wa Wizara hiyo kwa matumizi mazuri ya fedha za miradi katika utekelezaji na usimamizi mzuri nchini,na kuagiza iwe mfano katika miradi mingine yote ya serikali.

Mhe. Rais ametoa pongezi hizo baada ya kuridhishwa na kasi ya utekelezaji wa miradi ya maji nchini, ikiwemo utekelezaji wa Mradi Mkubwa wa Maji unaotumia chanzo cha Ziwa Victoria wa Tinde - Shelui aliozinduliwa tarehe 17 Oktoba,2023 katika Kijiji cha Kisonzo, Shelui-Singida.

Mhe. Rais ameiagiza Wizara ya Maji kuongeza kasi katika usambazaji wa maji kwa wananchi, kwani amefarijika kuona suala la maji linafanyiwa kazi na serikali na maji yanapatikana tofauti na awali alipokuwa anapokelewa katika ziara zake na ndoo na chupa za maji wananchi wakielezea tatizo la maji, hali ambayo haipo tena.

Katika kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maji, ameziagiza Mamlaka zinazohusika kuhakikisha hapatokei mkwamo kwa sababu zozote katika upatikanaji wa misamaha ya kodi inayostahili,ucheleweshaji wa vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni na utoaji wa vifaa bandarini









# Wizara ya Maji yakabidhi bonde la kilimi nzega kwa Wizara ya Kilimo

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua Mradi wa Uzalishaji wa Mbegu za Mazao ya Kilimo wilayani Nzega, akiwa ziara ya kikazi mkoani Tabora.

Akitoa taarifa ya mradi huo , Waziri wa Kilimo Mhe. Hussein Bashe (Mb) ameishukuru Wizara ya Maji inayoongozwa na Waziri wake Mhe. Jumaa Aweso (Mb) kwa kuikabidhi Wizara ya Kilimo Bwawa la Maji la Kilimi na Bonde la kilimo lenye ukubwa wa ekari 1,102 lililopo eneo la Uchama Wilayani Nzega kwa ajili ya kuanzisha Shamba la Mbegu.

Mhe. Bashe amesema kuanzishwa kwa Shamba hilo la Mbegu linalosimamiwa na Wakala wa Mbegu Nchini (ASA) kutachochea mpango wa Serikali wa kuwawezesha Vijana katika Sekta ya Kilimo.








## Milioni 500 kuondosha kero ya maji kata moja iliyosalia Nzega Vijijini - Waziri Aweso

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Maji katika Kata ya Puge Wilaya ya Nzega, Mkoani Tabora.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso ( Mb) amemhakikishia Mhe. Rais kuwa fedha hizo zitatolewa mapema iwezekanavyo ili kuwaondolea tatizo la maji wakazi wa Kata ya Puge.

Hatua hiyo inàjibu ombi la Mbunge wa Nzega Vijijini Mhe. Dkt. Hamis Kigwangala ambaye amesema ni kata moja tu ya Puge katika Jimbo lake ndio yenye changamoto ya uhaba wa maji.

Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameongea na wananchi wa eneo hilo akiwa katika ziara ya kikazi njiani Mkoani Tabora.



# Mradi wa maji wa Tinde Shelui sasa rasmi



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua mradi mkubwa wa maji unaotumia chanzo cha Ziwa Victoria eneo la Shelui mkoani Singida ukiwa na thamani ya jumla ya shilingi Bilioni 24.47 ikiwa ni fedha za mkopo nafuu kutoka Benki ya EXIM India.

Mradi huu kwa awamu ya kwanza ya utekelezaji ulikamilika tarehe 11 Agosti, 2023 kwa gharama ya shilingi Bilioni 24.47 na wananchi zaidi ya elfu arobaini wa vijiji vya Tinde mkoani Shinyanga na Shelui mkoani Singida tayari wanapata huduma ya majisafi na salama, na utekelezaji wa awamu ya pili utagharimu shilingi bilioni 16.2

Ujenzi wa mradi unasimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga (KASHWASA).
Hafla ya uzinduzi wa mradi huu imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Chama na Serikali, wakiwemo,Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb), Balozi wa India nchini Tanzania, Mhe. Binaya Srikanta Pradhan, Waziri wa Fedha na Mbunge wa Jimbo la Iramba Magharibi, Mhe. Mwigulu Nchemba (Mb). Maelfu ya wananchi wameshiriki katika tukio hili.



## “Mhe. Rais Samia, Tabora maji yapo” Waziri wa Maji Mhe. Aweso awahakikishia wananchi

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya ziara ya kikazi katika Mkoa wa Tabora ambapo ametembelea wilaya ya Igunga na Nzega katika miradi mbalimbali ikiwepo miradi ya maji.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) katika ziara hiyo ameeleza kuwa mkoa wa Tabora huduma ya maji ilikuwa changamoto sana lakini kwa sasa hali ni nzuri kwa sababu upatikanaji wa maji umefikia asilimia 98 mijini ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa katika kuhakikisha maji yanapatikana kwa asilimia 95 mijini na vijijini asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.



Ameongeza kuwa mkakati uliopo ni kuhakikisha maji kutoka ziwa Victoria yanafika katika Wilaya zote za Tabora ambapo hivi sasa ili kutimiza hilo wakandarasi wanafanya kazi site Sikonge, Urambo na Kaliua.

Amesema bayana na kumhakikishia Mhe. Rais kuwa yeye pamoja na timu nzima ya Wizara ya Maji hawatokuwa kikwazo kwa mkoa wa Tabora kupata majisafi na salama yenye kutosheleza.

# Mradi wa maji wa bilioni 8.7 wawekewe jiwe la msingi na Makamu wa Rais







Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wa maji wa Lugenge mkoani Njombe, ambao umefikia asilimia 82 ya ujenzi unaogharimu shilingi bilioni 8.7 na kutarajiwa kunufaisha zaidi ya wananchi elfu kumi.

Mhe. Dkt. Mpango amewahakikishia wananchi wa eneo la Ramadhani kuwa Serikali itaendelea kuwaletea maendeleo na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya kuwapatia wananchi majisafi, salama na yenye kutosheleza kwa asilimia 85vijijini na mijini asilimia 95 ifikapo mwaka 2025.
Ameielekeza Wizara ya Maji kukamilisha mradi wa maji wa Lugenge kama ulivyopangwa kwa kuwa fedha zipo na kufanyia kazi suala la kuwalipa fidia wananchi waliopisha maeneo ya miradi ya maji.

Kwa upande wake ,Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutenga fedha kiasi cha shilingi bilioni 8.7 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa chanzo cha Lugenge mkoani Njombe, na amewaahidi wananchi mradi huo utakamilika kwa wakati ifikapo mapema mwezi Februari, 2024.

## Makamu wa Rais asisitiza ulinzi wa mazingira, pamoja na vyanzo vya maji



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango amekemea tabia ya uharibifu wa mazingira na matumizi mabaya ya vyanzo vya maji, na kutaka kila mwananchi awe mlinzi wa mazingira.

Kufuatia hilo, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameitaka jamii kushiriki kubeba jukumu la kulinda na kutunza rasilimali za maji kwa faida ya matumizi mbalimbali ikiwemo kuzalisha Nishati ya umeme, Kilimo na matumizi mengine ya muhimu kwa kijamii,na kwamba kwa vyanzo vya maji vilivyoharibiwa na kukauka iwe fundisho kwa wengine kutoharibu rasilimali za maji.

Ametoa tahadhari hiyo ili jamii iendelee kulinda, kutunza na kuendeleza rasilimali za maji zilizopo katika kila kona ya nchi kwa maendeleo na ustawi wa jamii.

Akitoa salamu na shukrani, Mbunge wa Makete, Mhe. Festo Sanga ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa miradi ya maji inayotekelezwa katika wilaya hiyo yenye thamani ya shilingi bilioni 5.7, na hivi sasa wilaya ya Makete imekuwa ya kwanza kitaifa kwenye upatikanaji wa huduma ya maji kwa asilimia 99.
Makamu wa Rais yalifanya ziara ya kikazi mkoani mkoani Njombe kwa siku tatu ambapo Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) alikuwepo.

# Bilioni 42 zinatekeleza Miradi ya Maji Makambako - Aweso



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema Serikali ya Awamu ya Sita imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.2 kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji katika kata ya Mlowa, Kijiji cha Idofi mkoani Njombe.

Amesema hayo katika kijiji cha Idofi akiwa katika msafara wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdori Mpango anayefanya ziara mkoani Njombe.

Waziri Aweso amesema Wizara ya Maji haitakuwa kikwazo katika utekelezaji wa ujenzi wa miradi wa maji na kwamba fedha hizo shilingi bilioni 3.2 zitakamilisha mradi hu na kumuagiza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako kuanza mara moja utekelezaji wa mradi huo.

Sanjari na hilo, Waziri Aweso amemuhakikishia Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Mpango kuwa fedha shilingi bilioni 42 zinazotekeleza miradi mbalimbali ya maji katika mji wa Makambako zitakamilisha miradi yote kwa wakati ili kuwaondolea wananchi uhaba wa huduma ya majisafi.

Pamoja na hayo, Waziri Aweso ameridhia ombi la Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Mhe. Deo Sanga ambaye ameomba Wizara ya Maji kujenga Tenki kubwa la maji katika kata ya Mlowa, kijiji cha Idofi-Makambako ambapo kazi hiyo itatekelezwa kupitia mradi wa maji wa Mlowa wenye thamani ya shilingi bilioni 3.2.

Mhe. Sanga amempongeza Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) kwa kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Maji katika utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa Miji 28 ambapo Mkoa wa Njombe ni sehemu ya mradi huo.
Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Phillip Isdori Mpango yupo katika ziara ya kikazi ya siku tatu mkoani Njombe ambayo ameanza leo.

## Prof. Jamal atoa shule kuhusu mabadiliko ya tabianchi



Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu amesema ongezeko kubwa la watu na kukua kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi hapa nchini linatarajiwa ama linatishia kupunguza kiwango cha upatikanaji wa maji kwa mtu na kufikia mita za ujazo 883 ifikapo mwaka 2035.

Amesema hayo wakati wa warsha ya wadau kuhusu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na ustahimilivu katika maeneo ya nchi.
Prof. Jamal amesema hali hiyo inaweza kuwa mbaya zaidi kwa maeneo kame ya nchi kama hakutakuwa na mikakati mathubuti ya kukabiliana na tabianchi

Amesema kwa mkoa wa Dodoma ambao ni makao makuu ya nchi, kustawi kwa kuongezeka kwa idadi ya watu na kukua kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii kumeisukuma Wizara ya Maji kuendelea na utekelezaji wa mipango mbalimbali ili kuwezesha upatikanaji wa vyanzo vya maji safi.

Prof. Jamal amepongeza watekelezaji wa Mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na ustahimilivu katika nyanda kavu za kitropiki kupiitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Maji
Utekelezaji wa mradi utawawezesha kuunganisha wataalam wa Wizara ya Maji kupitia kituo Mahiri cha Rasilimali za Maji na watafiti wabobezi kutoka SUA, na nchi za Uingereza, India na Niger

# Mpanda-mradi wa maji wa miji 28 Mkandarasi yupo kazini, Mahundi





Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amesema  katika kuboresha huduma ya maji katika mji wa Mpanda, Serikali inatekeleza mradi wa maji wa miji 28 ambapo Mkandarasi anaendelea na kazi.

Mhe. Mahundi amesema hayo kwa niaba ya Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) wakati akishiriki katika majumuisho ya ziara ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi  (CCM) ndugu Daniel Chongolo mkoani Katavi

Ameongeza kuwa kwa miradi ya Mamba- Majimoto na Kapalamsenga - Karema Serikali inaendelea kusimamia na kufuatilia ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati  ili wananchi wapate huduma ya maji.

Ameainisha mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kutumia chanzo cha ziwa Tanganyika na taratibu za kumpata mtaalamu Mshauri zinaendelea na anatarajiwa kuanza kazi Desemba, 2023

Waziri Mahundi ameahidi kuwa tarehe 08 Oktoba, 2023 atafika kwenye mradi wa maji wa Ugalla uliopo wilayani Nsimbo kufuatilia utekelezaji wake na kutoa maelekezo kwa Mkandarasi wa mradi huo.

## Mkandarasi fanya kazi kwa saa 24 mradi wa Katambike-Mahundi







Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amemtaka Mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji wa Katambike kufanya kazi kwa saa 24 ili akamilishe mradi huo kwa wakati.

Mhe. Mahundi ametoa maelekezo hayo akiwa kata ya Ugalla, Mpanda mkoani Katavi  ikiwa ni mwitikio wa maelekezo ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Ndugu Daniel Chongolo aliyeelekeza mradi huo ukaguliwe ili kuona hatua za kuchukua na wananchi wapate huduma ya maji.

Waziri Mahundi amesema atarudi katika mradi huo, na endapo Mkandarasi  atashindwa kukamilisha ujenzi wa mradi  kwa muda uliopangwa, Wizara ya Maji itaendelea na utekelezaji wa kazi zilizosalia kwa utaratibu wa Force Account.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Mpanda Mhe. Jamila Kimaro amesema  atasimamia na kufuatilia  mradi huo ili kuweza kutoa mrejesho kuhusu utekelezaji wake kwa viongozi wa Wizara ya Maji.

# Hati za viwanja Bonde la Makutupora zifutwe - Mhe. Majaliwa



Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa ameagiza Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wizara ya Ardhi wafute hati zote zilizopimwa kwenye Bonde la Makutupora na kuwaondoa wavamizi waliojenga kwa sababu bonde hilo chanzo cha maji kwa jiji la Dodoma.

Ameliagiza Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wawafuatilie na kuwarejesha Dodoma watumishi 11 waliokuwa Halmashauri ya Jiji la Dodoma ili wajibu tuhuma za matumizi mabaya ya fedha, kupora maeneo ya wananchi na kugawa maeneo ya wazi.

“Watumishi wa Jiji la Dodoma ni Josephat Mafuru (aliyekuwa Mkurugenzi wa Jiji), Scorpion Philip, Lennis Ngole, Allen Mwakanjuki, Aisha Masanja, Agusta Primo, Azory William Byakanwa, Frezia Kazimoto, Premin Nzenga, Stella Komba na Thabiti Mbiyagi. Hawa ni wachache miongoni mwa wengi waliohusika kusababisha migogoro, watafutwe na waje kujibu tuhuma dhidi yao,” amesema.

Amesema kuwa Jiji la Dodoma litekeleze mapendekezo ya Kamati Maalum ya Uchunguzi kwa kufanya uhakiki wa hati pandikizi zote, litafute maeneo na kuwafidia wananchi wanaolidai Jiji na liwe limekamilisha utekelezaji ifikapo Januari 30, 2024.

“Halmashauri ya Jiji isitishe upimaji shirikishi wa asilimia 70 kwa 30 na sasa wabaini wananchi wote waliohusika na zoezi hilo ili walipwe ifikapo Januari 30, 2024.”

Kwa mujibu wa Taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kikao hicho kimehudhuriwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (SBU), Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, OR - TAMISEMI na Ardhi, Wakuu wa Mikoa hiyo sita, Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa Majiji hayo, Kamati Maalum ya Uchunguzi iliyoundwa na Waziri Mkuu ilibainisha kuwa mradi wa upimaji shirikishi wa asilimia 70 kwa 30 ulikuwa ni dhana iliyokuwa inatumiwa bila kufuata sheria.

# Mradi wa maji wa Murusagamba siku 30 kukamilika



Wizara ya Maji imetoa kiasi cha shilingi milioni 250 ili kuanza kutekeleza mradi wa maji katika kijiji cha Murusagamba, Ngara mkoani Kagera ambapo Mkuu wa wilaya ya Ngara Kanali Mathias Kahabi ameelekezwa kutumia nguvu kazi ya wafungwa kuchimba mitaro ukamilike katika siku 30 ili mradi uwe umekamilika na wananchi wakabidhiwe.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema hayo akiwa katika ziara ya kikazi katika kata Murusagamba, wilayani Ngara kufuatia agizo alilopewa na Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Dotto Biteko (Mb) kufanyia kazi changamoto ya upatikanaji wa maji katika eneo hilo.

Amesema kuongezeka kwa idadi ya watu katika kijiji cha Murusagamba kumesababisha huduma ya maji kutotosheleza hivyo mradi huo utawekewa miundombinu mipya ili maji yafike kwa wananchi.

Waziri Aweso amemuagiza Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) mkoa wa Kagera kutangaza mradi wa maji wa kijiji cha Ntanga wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 700 ili wananchi wa kijiji hicho waanze kupata maji.

Pamoja na hayo, amemtaka mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji wa Kumubuga kuripoti katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kutoa maelezo ya lini atamaliza mradi anaotekeleza kutokana na kuchelewa kwa mradi huo.

Wakati habari hii inachapishwa, tayari mradi huu unatoa huduma kwa wananchi

# Prof. Jamal akitaka Chuo cha Maji kuongeza somo la ujasiriamali





Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu ameutaka uongozi wa Chuo cha Maji na Bodi ya Chuo hicho kukiimarisha Chuo katika utafiti,ushauri na mafunzo ya ujasiriamali ili kukiimarisha Chuo,Wakufunzi na kuendelea kuzalisha wahitimu walio bora zaidi.

Katibu Mkuu Prof. Katundu amemuwakilisha Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) katika Mahafali ya 47 ya Chuo cha Maji yaliyofanyika katika Ukumbi wa Mlimaji City Jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia miradi ya uendelezaji wa miundombinu ya Chuo cha Maji cha Jijini Dar es Salaam, Prof. Katundu amesema ukarabati na ujenzi wa miundombinu takribani 32 ya majengo ya Utawala,Maktaba,Mabweni na Madarasa yanayogharimu shilingi bilioni 7.5 kutoka serikali kuu yatakamilika kwa wakati.

Aidha Prof. Katundu amemuagiza Mkuu wa Chuo cha Maji,Dkt. Adam Karia kuweka utaratibu wa mafunzo kwa vitendo kwa Vijana 682 waliohitimu kwa kuwapeleka katika Mamalaka za Maji nchini kupata ujuzi katika fani zao baada ya masomo ya darasani.

Pamoja na hayo amekitaka chuo kusimamia kwa nguvu jukumu la kuwaandaa vijana katika fani mbalimbali za Sekta ya Maji.





# Mradi wa Maji wa Miji 28 Kukamilika kwa Wakati – Aweso



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amehawahakikishia Watanzania kuwa mradi wa maji wa miji 28 utakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa mwaka 2025.
Mhe. Aweso amesema hayo akiwa jijini New Delhi nchini India alipofanya mazungumzo na viongozi wa makampuni ya wakandarasi wanaotekeleza mradi huo .
Waziri Aweso ambaye yupo nchini India katika ziara ya Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya mazungumzo hayo akiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu na Mwakilishi wa Balozi wa Tanzania nchini India Bwana Deo Dotto na Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali za Maji Robert Sunday.
Akizungumza na Wakandarasi hao pamoja na Mkandarasi Mshauri na mwakilishi wa Benki ya Exim ya India ameeleza jinsi Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alivyowezesha kukamilika kwa michakato ya Mradi huo kuanza baada ya kuchukua muda mrefu na kuhimiza kazi ifayike vizuri ikiwa ni kurejesha shukrani kwa kiongozi wa nchi na kutimiza ufanikishaji wa malengo yake ya "Kumtua Mama Ndoo Kichwani".

Ameahidi ushirikiano katika hatua zote katika kipindi cha utekelezaji wa mradi huo, Pamoja na hilo wadau wameshukuru uongozi wa Wizara ya Maji kwa kuridhia kukutana nao na kusikiliza changamoto zao na kutoa majibu.

## Visima 450 kuchimbwa Kibiti na Simanjiro

Katibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu amesaini mkataba wa makubaliano na Asasi ya Mtandao wa Msaada (Global Aid Network) ya Canada kuhusu kazi ya uchimbaji wa visima vya maji vipatavyo 450.

Hafla ya utiaji Saini imefanyika Jijini Dodoma na Asasi hiyo imewasilishwa na Meneja Uendeshaji na Ufundi Bw. Stephen Thomson
Visima hivyo vitachimbwa Kibiti na Simanjiro, na kila mwaka vitachimbwa visima 90 kwa kipindi cha miaka mitano ya mkataba. Urefu na kiwango cha uchimbaji kwenda chini itakuwa mita 200.

Kazi hii itafanywa kitaalamu na kufuata taratibu za Serikali kwa kushirikisha Bodi za Maji za Mabonde katika maeneo husika, na Maabara za Ubora wa Maji ili kujua ubora wa maji kabla ya kutoa huduma kwa wananchi.



# Mhandisi Limbe awatambua wateja kwa ushirikiano wao katika huduma ya maji

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi (MUWSA Mhandisi Kija Limbe, amewashukuru wateja na wadau wote wa MUWSA kwa ushirikiano mkubwa wa dhati katika kuhakikisha mamlaka anayoiongoza inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa wananchi.

Mhandisi Limbe ameyasema hayo katika hafla fupi mjini Moshi wakati wa kuhitimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja 2023 ambapo kwa niaba ya Wizara ya Maji ametunuku vyeti vya shukrani kwa wawakilishi wa wateja wa huduma ya maji wa mjini Moshi.

“ Ninawashukuru sana wateja wetu kwa kuendelea kuchangia huduma zinazotolewa na Mamlaka yetu yam aji, na tunawaahidi kuendelea kuwapa huduma dhabiti, bora na endelevu .” Mhandisi Limbe ametoa ahadi hiyo.

MUWSA imewatunuku vyeti wateja wake watatu ambao ni kampuni ya bia ya Serengeti Breweries Limited, kampuni ya magari ya Rajinder Motors LTD pamoja na Chuo cha Usimamizi wa Wanyama pori Mweka.

Wateja hao wamepatikana kwa kigezo cha ulipaji wa Ankara kwa wakati pamoja na ushirikiano mkubwa unaotolewa na taasisi hizo katika Sekta ya Maji.

Akizungumza kwa niaba ya wateja waliotunukiwa vyeti, Mwakilishi kutoka kampuni ya Rajinder Motors LTD Bi. Laila Kanakis amesema,”Tunawashuru MUWSA kwa kuthamini mchango wetu nasi tunaahidi kuendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa MUWSA”.

Mkurugenzi Mhandisi Limbe amewaasa baadhi ya wananchi wanaohujumu miundo mbinu ya serikali ikiwemo wizi wa mifuniko ya chemba za majisafi na majitaka pamoja na wizi wa Dira za maji kuacha mara moja kwani wanafifisha jitihada za serikali za kufikisha huduma ya maji kwa wananchi.

Amewataka wananchi kushirikiana na Mamlaka ya Maji kwa ulinzi na kutoa taarifa kupitia ofisi za Mamlaka au Jeshi la Polisi wanapowabaini wahujumu wa miundombinu kwa sababu huduma ya maji ni maendeleo ya wananchi na nchi.

Amesema zawadi nono itatolewa kwa yeyote atayefanikisha kukamatwa kwa wahujumu wa miundo mbinu hiyo na taarifa atakazotoa zitakuwa siri.





# Mzee Msekwa, Spika mstaafu apongeza utendaji katika Sekta ya Maji

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Bi. Neli Msuya amemtembelea Spika Mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe Pius Msekwa katika makazi yake Nansio, Wilayani Ukerewe ikiwa pia ni siku maalum ya kumbukizi ya miaka 24 ya kifo cha Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.


Kaimu Mkurugenzi Bi. Neli akiwa Ukerewe Pamoja na kumjulia hali mzee Msekwa, amekagua ufanisi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Nebuye unaohudumia wakazi wa Mji wa Nansio..

Amemueleza Mhe. Msekwa hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Wizara ya Maji kupitia MWAUWASA za kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Mwanza na hususan kwa mji wa Nansio.

"Tunatarajia kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma ya maji katika mji wa Nansio, tunatekeleza azma ya Rais wetu, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Waziri wetu wa Maji Mhe. Jumaa Aweso ya kumtua Mama wa Nansio ndoo ya maji kichwani," Bi. Neli amesema

Ameongeza uwezo wa mtambo wa kuzalisha maji wa Nebuye ni lita milioni 8.6 kwa siku na hivyo kinachofanyika sasa ni kutanua mtandao sambamba na kuhamasisha wananchi kujiunga na mfumo wa maji.

Mheshimiwa Msekwa ameridhishwa na hatua zinazochukuliwa na amepongeza Serikali kwa dhamira yake ya kuboresha upatikanaji wa maji kwa wakazi wa Nansio.





Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Msekwa amemzawadia Mkurugenzi Neli nakala ya kitabu alichokisaini cha 'Uongozi na Utawala wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere" cha Mwaka 2012 ambacho amekiandika.

# Serikali yatoa bilioni 70 kuimarisha huduma ya maji Mwanza




Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. CPA Amos Makalla amesema Serikali inatambua changamoto ya upungufu wa huduma ya maji inayowakabili wananchi wa jiji la Mwanza na hatua zinachukuliwa ikiwemo ujenzi wa miradi mbalimbali ya maji.

"Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuletea fedha zaidi ya shilingi bilioni 70 ambazo zinajenga mradi mkubwa wa maji eneo la Butimba, mradi wa upanuzi wa chanzo kilichopo cha Capripoint na mradi wa upanuzi wa mtandao wa majisafi kwenye maeneo mbalimbali ili kupunguza adha ya upungufu wa maji sambamba na kutanua wigo wa upatikanaji wa maji kwa wananchi ambao bado hawajafikiwa," Mhe. Makala amesema

Amesema mradi wa maji wa Butimba tayari umeanza kazi kwa majaribio na kukamilika tarehe 31 Oktoba,2023 na Serikali imetangaza kumpata Mkandarasi atakayepewa kazi ya kutanua chanzo cha Maji cha Capripoint .

"Sote hapa ni mashuhuda; Mwanza kulikuwa na changamoto ya maji lakini kwa sasa tunajionea shughuli zinazoendelea ikiwemo hii ya ulazaji wa mabomba hapa Ilemela lakini pia na wilaya nyingine ikiwemo Nyamagana na Magu," Mhe. Makala ameainisha.

Amewataka wananchi kutoa ushirikianokwa Mamlaka ya Maji Mwanza (MWAUWASA) wakati huu ikitekeleza miradi katika maeneo mbalimbali na pia amempongeza Kaimu Mkurugenzi wa MWAUWASA Bi. Neli Msuya kwa kujitoa katika kazi kuhakikisha miradi inajengwa kwa kasi.

"Kwa muda mchache Mkurugenzi huyu ameonyesha ni msikivu anatembelea wananchi na kutatua changamoto zinazowakabili na anasimamia miradi na tunashuhudia inakwenda kwa kasi. Neli wewe ni mwanamama ninaimani utawahurumia wanamama wenzako wapate maji," RC Makala amesema.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Bi. Neli Msuya amesema MWAUWASA inaendelea na ujenzi wa miradi midogo ili kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo mbalimbali ya jiji la Mwanza.



# Ukaguzi wa Bwawa la Nsekwa Wafanyika

Mkuu wa Wilaya ya Mlele, Mh Majid Mwanga akiwa na Mkurugenzi wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa Bi. Grace Chitanda katika ukaguzi wa bwawa la Nsekwa lililopo Wilaya ya Mlele, Mkoani Katavi. Lengo likiwa kuhakikisha bwawa hilo linahifadhiwa kwa mujibu wa Sheria, pia watu wote wanaofanya shughuli za kibinadamu ndani ya eneo hifadhiwa wanaondolewa mara moja.

Mkurugenzi Chitanda ametoa taarifa kuwa bwawa hilo ndio chanzo cha uhakika cha maji ambacho kitaondoa tatizo la muda mrefu la uhaba wa maji katika mji wa Inyonga na viunga vyake.



# Ifakara: Mradi wa maji wa Mbingu sasa ni maji bombani

Mradi wa maji wa Mbingu - Igima sasa unanufaisha zaidi ya wananchi elfu 36 katika vijiji saba katika kata za Mbingu na Igima, Tarafa ya Mgeta Halmashauri ya Mlimba wilayani Kilombero.

Kazi zilizofanyika kwa awamu ya kwanza ni pamoja na Ujenzi wa dakio la maj , ulazaji wa bomba za maji zenye urefu wa mita 22,313, ujenzi wa chujio la maji (sedmentation tank), ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa lita 250,000 juu ya ardhi na ujenzi wa idadi vituo vya kuchotea maji wananchi 20.

Kamati ya Bodi ya Miradi na Ufundi ya Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) imekagua mradi huo ikiendelea na ziara mkoani Morogoro.
Kazi katika mradi huo zinaendelea kwa awamu ya pili na tatu. Gharama za mradi mpaka kukamilika kwake ni shilingi 3,431,773,992.



# Prof. Katundu ataka wananchi wapate maji mapema Same



Katibu Mkuu Wizara ya Maji Prof. Jamal A. Katundu amekagua Mradi wa Maji Same – Mwanga- Korogwe na kusisitiza ratiba ya ujenzi lazima ipewe kipaumbele ili kufikisha huduma ya majisafi ya uhakika kwa wananchi.

Prof. Katundu katika ukaguzi huo ameelekeza ;
Mradi huo ni lazima ukamilike ndani ya muda uliopangwa ili kufanikisha huduma ya majisafi kwa jamii kwa haraka.
Kuhusu vifaa vya Mkandarasi, amesema mkandarasi wa mradi kampuni ya MS Advent inatakiwa kukusanya vifaa vyote muhimu vinavyohitajika kwa ajili ya ujenzi ili kuwa na maendeleo ya ujenzi yasiyokatizwa na uzingatiaji wa ratiba ya mradi.

Prof. Katundu kuhusu madeni yanayodaiwa ameeleza kuwa Serikali itadumisha ushirikiano wa uwazi na utamaduni wa usawa kwa wakandarasi wote wa mradi na Wahandisi washauri. “ Malipo yote ambayo yanadaiwa na wakandarasi na wahandisi washauri yatalipwa mara moja na Serikali. Hatua hii sio tu itasaidia maendeleo ya mradi lakini pia itakuza moyo wa ushirikiano na uaminifu kati ya Serikali na washirika wake wa mradi” Prof. Katundu ameainisha.

Mhandisi Abbas Pyarali, wa Wizara ya Maji, ambaye ni Kiongozi wa Timu ya Uratibu wa Mradi huo amesema maelekezo yote yamepokelewa na yatafanyiwa kazi ipasavyo kwa kuzingatia weledi na umakini ili kufikia lengo la Serikali la kuwapatia wananchi huduma ya uhakika ya majisafi na salama.

# Singida: Huduma ya maji yafika Manga

Wakati wa Wiki ya Huduma kwa Wateja Duniani 2023, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) kwa kushirikiana na asasi ya misaada ya Direct Aid Society imefanikisha huduma ya majisafi eneo la Manga, katika Manispaa ya Singida.

Kazi ya uchimbaji mtaro imefanyika kwa umbali wa mita 5800 na huduma imefika katika shule ya Msingi ya Arafa iliyopo eneo la Manga.
Kazi hiyo imegharimu kiasi cha shilingi milioni 88.





# Kazi Bwawa la Ilambambasa, Maswa sasa asilimia 90





Mradi wa ukarabati wa bwawa wa Ilambambasa wilayani Maswa mkoa wa Simiyu umefikia asilimia 90 ya utekelezaji na unatarajiwa kuwanufaisha wananchi zaidi ya elfu tisa wa vijiji saba vya Mwabusalu, Igungulyankoma, Mwakabeya, Mwamitumaye, Mbugamita, Senani, Ilambambasa na idadi ya mifugo zaidi ya elfu 14.

Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria inafanya kazi ya upanuzi wa bwawa hilo kwa thamani ya shilingi milioni 900.
Serikali inafanya kazi katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo ya vijijini inafika asilimia 85 mwaka 2025 na mradi huu ni moja ya miradi mikubwa itakayoleta matokeo ya moja kwa moja kwa wananchi na wanufaika wengine wanaotegemea bwawa hilo.

# Vijiji 12, 314 tayari maji bombani, vingine 2, 643 ndani ya miezi 24 - Aweso

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema kufuatia matokeo ya Tathmini ya Hali ya Upatikanaji wa Maji Vijijini katika Vijiji 12,314 iliyofanywa na Wizara ya Maji, na kusababisha kuanzishwa kwa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA), Wizara ya Maji imefanikiwa kufikisha huduma ya maji katika vijiji 9,671 na vijiji vilivyobaki 2,643 vitakamilika ndani ya miaka miwili ijayo kuanzia sasa 2023

Mhe. Aweso amemuhakikishia Mhe. Rais Samia kuwa Vijiji vyote vilivyobaki vitapata maji na Wizara ya Maji itahakikisha visima na mabwawa yanachimbwa katika maeneo yote yenye uhitaji.
Akizungumzia kuhusu utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji unaotumia chanzo cha ziwa Victoria, Mhe. Aweso amemuhakikishia Mhe. Rais Samia mradi huo unatekelezwa kwa kasi.

Aidha Mhe. Aweso amesema mradi mkubwa wa maji wa Miji 28 unaendelea kutekelezwa, ikiwa ni sehemu ya matunda ya ziara yake ya kikazi nchini India na kwamba kukamilika kwa mradi huo kutaondoa kabisa uhaba wa maji katika maeneo yote unapotekelezwa.

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema hayo aliposhiriki Maadhimisho ya Miaka 60 ya mkoa wa Singida katika uwanja wa Bombadia, ikiwa ni sehemu ya ziara ya siku tatu ya kikazi iliyofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan mkoani Singida.



Mkuu wa Wilaya ya Chemba Mhe George Mongela ameongoza kikao cha wataalam kutoka Wizara ya Maji kuhusu utunzaji na usimamizi wa Kidakio cha maji kwenye Bwawa la Farkwa litakalokuwa na mita za ujazo milioni 470 ambao litawanufaisha wakazi wa Chemba, Bahi, Chamwino na jiji la Dodoma.

Kikao hicho kilikuwa na lengo la kumtambulisha Mtaalamu Mshauri, Geo Network Limited ambaye atafanya kazi hiyo katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

Miongoni mwa kazi zitakazo fanywa ni pamoja na utafiti wa eneo la kidakio cha maji kwenye eneo la bwawa na utunzaji wa mazingira ikiwemo upandaji wa miti rafiki wa maji ili kufanya uendelevu wa matumizi bwawa hilo.

Wataalamu hao wametakiwa kuwashirikisha wananchi katika eneo husika. Aidha, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, amesisitiza ujenzi wa bwawa ukamilike kwa wakati kama ulivyopangwa.





# Dar es salaam: Mivumoni huduma ya maji kuwafikia zaidi ya 250

Wananchi mbalimbali wamejitokeza katika ofisi za Mkoa wa kihuduma za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) Mivumoni kupata vifaa vya maunganisho mapya ya huduma ya majisafi baada ya kukamilisha taratibu za awali za kuomba huduma na wanategemea kuhudumiwa kupitia mradi wa maji wa Chuo kikuu hadi Bagamoyo uliokamilika mapema Mwezi Machi,2023.

Meneja wa DAWASA -Mivumoni ndugu Gilbert Massawe akiongea wakati wa kukabidhi vifaa hivyo amewaeleza wakazi hao kuwa kila mmoja atapata huduma na kuwasihi waendelee kujitokeza kadri ya utaratibu utakavyopangwa ili kuendelea kuchukua vifaa vya maunganisho.

“Leo tutagawa vifaa kwa wananchi takribani 250 ambao walishakwisha fanya malipo yao, hii inaashiria kuwa wanaenda kupata huduma ya Majisafi kutoka DAWASA” Massawe ameeleza.

“Nitoe wito kwa wateja kuendelea kuongeza ushirikiano kwa Mamlaka na pindi wanapopata huduma kuanza kulipia ankara kwa wakati Ili wananchi wengine katika maeneo tofauti wapate huduma pia” Masawe ameainisha

Ndugu Ramadhan Maulid mkazi wa Mivumoni ameishukuru DAWASA kwa kuwapatia vifaa vya maunganisho na sasa wanapata uhakika wa huduma ya maji waliyoisubiri kwa muda mrefu.

“Maeneo yetu kwa muda sasa tulikosa huduma ya maji, tunapongeza jitihada za DAWASA katika ukamilishaji wa miradi lakini zaidi kuwaunganisha wateja na huduma, leo hii tuna uhakika tunaenda kupata huduma ya maji kila mmoja katika makazi yake” Maulid ameeleza.

Wakazi watakaopata huduma ya majisafi ni kutoka maeneo ya Kilimahewa ,Salasala, Goba, Madale, Nyakasangwe, Muungano, Tegeta A, Mivumoni, Kulangwa, Kinzudi, Kilimahewa Juu na Boko Dovya.







# Aweso aitaka DUWASA ndani ya mwezi mmoja kumaliza mradi wa Nzuguni



Waziri wa Maji Mhe Jumaa Aweso(Mb) ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) kukamilisha mradi wa maji wa Nzuguni ndani ya mwezi mmoja.
Amesema hayo jijini Dodoma akiwa na watendaji wa Wizara ya Maji na viongozi wa Mkoa wa Dodoma.
Waziri Aweso amemuelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA Mhandisi Aron Joseph kukamilisha kazi hiyo na katika siku saba ili wananchi waanze kupata huduma ya majisafi, wakati kazi nyingine za ukamilishaji zikiendelea. Pia, amewataka wakandarasi kufanya kazi kwa saa 24.
Waziri Aweso ameipongeza DUWASA kwa kazi kubwa inayofanya katika kuhakikisha huduma ya maji inapatikana baada ya ongezeko la shughuli mbalimbali ikiwamo baada ya makao makuu ya Serikali kuhamia Dodoma.
Waziri Aweso ameainisha kuwa kazi hiyo ni juhudi za muda mfupi kwa mradi wa maji wa Nzuguni awamu ya kwanza.
Amesema upo asilimia 93 ambapo kazi iliyobakia ni ndogo na itakamilishwa ndani ya kipindi i cha mwezi mmoja.
Mradi wa maji Nzuguni utaongeza asilimia 11.7 na utahudumia wakazi zaidi ya 75,000 katika maeneo ya Nzuguni , Kisasa Nyumba 300, Ilazo na Swaswa.

Waziri Aweso amesema kuwa DUWASA imeanza utekelezaji wa mradi wa uchimbaji wa visima vitano kwa awamu ya pili katika eneo la Nzuguni lengo likiwa kuongeza maji kwa asilimia zisizopungua 15.
Ametaka kazi ya kuchimba kisima cha mita 300 kwa mara ya kwanza katika Jiji la Dodoma kama ilivyoelekezwa na wataalamu kuwa kuna uwezekano wa kupata maji mengi zaidi ya kumaliza tatizo la maji ianze mara moja na katika miezi miwili majibu ya kazi hiyo yapatikane.

Waziri Aweso amesema Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Mhe Dkt Samia Suluhu Hassan inawajali wananchi na wakazi wa Dodoma pamoja na uwepo wa mipango ya muda wa kati ikiwamo ujenzi wa Bwawa la Farkwa na mpango mkubwa wa muda mrefu wa kutumia chanzo cha maji cha ziwa Victoria bado mipango ya muda mfupi kama itaendelea kwa kasi ili kunusuru hali halisi ya changamoto ya huduma ya maji katika jiji la Dodoma.

# Mradi wa Usanifu wa Bwawa la Farkwa Wasainiwa, litajaza maji zaidi ya lita milioni 400



Wizara ya Maji imesaini mkataba wa mwaka mmoja na Kampuni ya SU-YAPI Engineering Consulting Inc. kwa ajili ya kufanya kazi ya usanifu wa ujenzi wa Bwawa la Farkwa litakalojengwa katika Wilaya ya Chemba, ambalo litanufanisha wakazi wa Wilaya za Chemba, Chamwino,Bahi na Jiji la Dodoma.

Mkataba umesainiwa tarehe 23 Oktoba, ikiwa ni awamu ya kwanza, mradi ambao utagharimu kiasi cha shilingi Bilioni 312 kwa ujenzi wa Bwawa lenye ujazo wa lita za maji milioni 440.

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameshuhudia hafla hiyo na amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 312 ili kuondosha tatizo la maji katika Wilaya nne za mkoa wa Dodoma ili wakazi wake wapate majisafi, salama na yenye kutosheleza.





Mhe. Aweso amewahakikishia wananchi wa Wilaya ya Chemba kuwa Wizara ya Maji itatekeleza mradi huo kwa kuwashirikisha wananchi ili wawe sehemu ya mradi na ujenzi ukamilike kwa wakati kama ilivyopangwa na Serikali.

Kwa Upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mhe. Jackson Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, ameishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia kwa kujitoa na kupeleka fedha kiasi cha shilingi bilioni 312 kwa ajili ya ujenzi wa Awamu ya kwanza ya Bwawa la Farkwa.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule akiongea katika hafla hiyo amewaomba wananchi wa Wilaya ya Chemba kuwa na imani na serikali yao kwa kuwa tatizo la upatikanaji wa maji linaisha kwani Serikali imedhamiria kumaliza kabisa changamoto ya uhaba wa maji kwa wakazi wa Wilaya ya Chemba.

# Mwanza: Huduma ya majisafi kuimarika zaidi

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), Bi. Neli Msuya amesema huduma ya majisafi inaendelea kuimarika kadri miradi iliyopangwa na Serikali inavyoendelea kukamilka.



Amesema hayo wakati wa mapokezi ya shehena ya mabomba ya ukubwa wa inchi 12 kwa ajili ya kuendeleza mtandao wa usambazaji maji kwa umbali wa kilomita 6.9 kutoka eneo la Buswelu hadi Ilalila, Wilayani Ilemela.

"Niwasihi wananchi waendee kushirikiana nasi MWAUWASA; miradi ya kuboresha huduma ya maji inaendelea kutekelezwa maeneo mbalimbali na kadri inavyokamilika ndipo huduma nayo inaendelea kuimarika na si suala la siku moja; maendeleo ni hatua," Bi. Neli amesema.

Ameongeza kwa sasa MWAUWASA itafungua Madawati ya Huduma kwa Wateja kwa ajili ya kurahisisha ushirikishwaji na mawasiliano kwa wananchi, kufikisha elimu na kutoa taarifa za hatua mbalimbali za ujenzi wa miradi kwa kushirikiana na viongozi wa maeneo husika.



"Tunashukuru viongozi na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia wakati huu tukitekeleza miradi; niwasihi tu msichoke kila tunapowaita ili kuwapa mrejesho," Bi. Neli amesema.

Amesisitiza kuwa miradi hiyo inafadhiliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia mia moja ikiwa ni jitihada za Rais. Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi.

Amesema mradi wenye thamani ya shilingi bilioni 4.7 utafikisha huduma ya maji kwenye maeneo ambayo hayakuwa na mtandao toshelevu hapo awali na pia kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwenye maeneo yaliyo na changamoto.

Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 53 na mtandao wa bomba umbali wa kilomita 14 umelazwa na matarajio ni kukamilisha mradi ifikapo Desemba 15.

"Tunafanya kazi kwa kasi ili Desemba 15 tuwe tumekamilisha mradi hasa ikizingatiwa kwamba tunaelekea kwenye msimu wa mvua nasi hatutaki kuwa na kikwazo kwani fedha tayari tunayo, nguvu kazi ipo ya kutosha na tunashirikiana kwa karibu na viongozi wa maeneo husika na jamii," Bi. Neli amesema.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Shibula, Mhe. Swila Dede ameishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi kwa mradi wa maji ambao amesema utaboresha huduma ya maji kwa wananchi wa kata hiyo.

Naye, Diwani wa Kata ya Buswelu, Mhe. Sarah Ng'wani amesema kata yake ilikuwa ikikakabiliwa na upungufu wa huduma ya maji hata hivyo anasema kupitia jitihada za Serikali zinazoendelea tayari kuna ahueni ya upatikanaji wa maji.

"Tunaishukuru Serikali kupitia Waziri wa Maji Mhe. Aweso , kwa kweli anasema na kutenda. Alipita hapa Mhe. Aweso na alituahidi kufanyia kazi changamoto hii na hapa tumeshuhudia yakitendeka. Tunasema ni Wizara inayotekekeza inayosema, ikiwemo ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa kivitendo," Mhe. Sarah amesema

# Kamati ya Bunge yawataka wadau kushirikiana kutunza vyanzo vya maji hapa nchini

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira imewataka wadau wote wa Sekta ya Maji kushirikiana ili kuhakikisha vyanzo vya maji vinalindwa, vinatunzwa na kuendelezwa.

Wito huo umetolewa na Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Felix Kavejuru (Mb) wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua bwawa la Mindu linalotarajiwa kuboreshwa ili kuwa na uwezo wa kuhifadhi maji zaidi na kuwezesha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama yenye kutoshekeza kwa wakazi wa Manispaa ya Morogoro.

Amesema uhai wa binadamu kwa kiasi kikubwa unategemea maji na ili maji yapatikane kwa uhakika lazima sekta zote zishirikiane. Amezitaja miongoni mwa sekta hizo kuwa ni pamoja na sekta ya ardhi, misitu, mazingira, sekta ya kilimo na sekta nyingine mtambuka ambazo kwa njia moja au nyingine zinahusika moja kwa moja nab huduma ya maji.

Kwa upande wa jamii inayozunguka vyanzo vya maji amesisitiza utoaji wa elimu itakayowezesha wananchi kutambua umuhimu wa vyanzo vya maji na hivyo kushiriki katika kuvilinda na kuviendeleza kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amesema Wizara ya Maji imejipanga kuhakikisha vyanzo vyote vya maji nchini vinalindwa ili kuwezesha upatikaji wa huduma ya maji kwa kila Mtanzania. Amekiri kuwepo na changamoto ya uvamizi wa vyanzo vya maji sehemu mbalimbali ikiwemo vyanzo vya bwawa la Mindu hali ambayo imepekekea kina cha maji kupungua na hivyo kutishia uendelevu wa Bwawa hilo, na kusisitiza jamii inashirikishwa ili maji yaendelee kuwepo kwa kuepuka uharibifu. Amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu fedha itolewe kwa ajili ya ukarabati wa bwawa hilo.

Awali akitoa taarifa ya ukarabati wa Bwawa hilo Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) Mhandisi Tamimu Katakweba amesema serikali inatarajia kutumia kiasi cha bilioni 225 za kuboresha huduma ya Majisafi na usafi WA mazingira katika mji morogoro ikiwamo ukarabati wa tuta la bwawa hilo ambalo ni chanzo pekee cha uhakika kwa huduma ya maji kwa wakazi wa Manispaa ya Morogoro.











Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Dkt. Moses Kusiluka akiwa katika ziara katika mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma akiwa ameambatana na Makatibu Wakuu. Miongoni mwa maelezo aliyopewa ni ujenzi wa miundombinu ya majitaka kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) Mhandisi. Aron Joseph

# Isimani – Kilolo mambo safii









Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa (IRUWASA) imekagua utekelezaji wa mradi wa maji wa Isimani – Kilolo ambao unathamani ya shilingi bilioni 9.2

Mradi huo ujenzi wake umefikia asilimia 95. Ni mradi wa vijiji 29, vijiji 24 vikiwa katika Jimbo la Isimani na vijiji vitano vikiwa Jimbo la Kilolo.

Fedha ya utekelezaji wa mradi imetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili wananchi katika vijiji hivyo wapate huduma bora ya majisafi, salama na yenye kutosheleza

# Kamati ya Bunge ya Maji na Mazingira yataka msukumo zaidi kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda




Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira imeitaka Serikali kuongeza msukumo wa fedha kwa wakati ili kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda.

Bwawa hilo linalenga kuwezesha uhai wa kudumu wa mto Ruvu kwa kuhifadhi maji wakati wa masika na hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwa siku 365, mikoa hiyo inategemea maji ya mto Ruvu kama chanzo kikuu cha huduma ya maji.

Wito huo umetolewa mjini Morogoro kupitia kwa Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Felix Kavejuru (Mb) wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa bwawa la Kidunda. Amesema mradi huo unaenda kuchochea uchumi wa nchi nzima katika maeneo tofauti tofauti hivyo ni mradi muhimu wa serikali na wenye uzito.

“Huu mradi unaenda kuchochea maendeleo ya Taifa. Tumeambiwa utazalisha umeme megawati 20 ambazo zitasaidia vijiji vinavyozunguka mradi na kuongeza uzalishaji kwenye gridi ya Taifa. Mradi utachochea kilimo, utachochea ufugaji, pia kukuza viwanda. Haya manufaa ni makubwa kwa serikali, wasimamizi na watekelezaji wa mradi wahakikishe wanatimiza wajibu wao kwa viwango vinavyo hitajika” Mhe. Kavejuru amesema.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu fedha zitolewe ili kutekeleza mradi huo. Amesema mradi huo ni wa kimkakati na imekuwa ni ndoto ya Muda mrefu ya Wzara ya Maji kuhakikisha inawezesha upatikanaji wa majisafi kwa wananchi wa mikoa nufaika.

Mhe. Mahundi amepokea maombi ya wananchi wa kijiji cha Mkulazi kupitia Mbunge wa eneo hilo Mhe. Hamis Shaban (Babu Tale) ya kutaka wananchi wa maeneo yanayozunguka mradi wapewe kipaumbele katika ajira za utekelezaji wa mradi.

Amemuagiza Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mhe. Rebeca Nsemwa kuhakikisha ndani ya wiki moja anakutana na kufanya kikao na mkandarasi kampuni ya Sinohydro Cooperation Ili kubaini iwapo ajira hizo zinatolewa kwa wananchi husika.

Mradi wa ujenzi wa bwawa la Kidunda unatarajia kugharimu shilingi bilioni 329 na kukamilika mwaka 2026.



# Watumishi wa Makonde wapigwa jeki ya vifaa vya kazi na Serikali





Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde imekabidhiwa vyombovya moto, Pikipiki 12 kwa ajili ya kuwahudumia wananchi katika huduma ya maji.
Mkuu wa Wilaya ya Newala Mh. Alhaj Rajab Kundya amekabidhi vyombo hivyo vya usafiri kwa mafundi wa mamlaka hiyo leo.
Amesema kuwa pikipiki hizo zitasaidia kuwafikia wateja mapema na kutoa majibu ya changamoto kuhusu huduma ya majisafi, na amewataka watumishi watakaotumia vyombo hivyo kuwa waangalifu, makini na kuwa na nidhamu.
Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Makonde, Mhandisi Francis Bwire amesema kuwa mamlaka hiyo itaendelea kununua vyombo vya usafiri hasa pikipiki ili kuweza kumaliza changamoto katika utoaji huduma.
Hafla ya makabidhiano imehudhuriwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji ya Makonde, Bi. Isabella Chilumba. Vyombo hivyo vilivyokabidhiwa ili kuwahudumia wananchi vinathamani ya shilingi milioni 45.6

## Tandahimba: Kazi ya kusogeza zaidi huduma ya majisafi kwa wananchi

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makonde inaendelea kufanya kazi ya kuwahudumia wananchi kwa upanuzi wa mtandao wa usambazaji maji mjini Tandahimba.

Lengo mahususi ni kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi wengi na kwa urahisi katika makazi yao, ili wasipoteze muda mwingi katika kufuata huduma hiyo.

Kufuatia umuhimu wa kazi hiyo Mamlaka ya Maji Makonde imezindua programu maalumu ya kusogeza huduma ya maji kwa wananchi ambapo Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba Mh. Kanali Patrick Sawala, amezindua jambo hilo kwa kupokea bomba za usambazaji maji zenye urefu wa kilomita tatu na vyombo vya moto (Pikipiki) tano zilizotolewa na Serikali.

Kanali Sawala amesema kazi hiyo ni azma ya serikali ya "kumtua mama ndoo ya maji kichwani" na ameshukuru kwa hatua hiyo kwa niaba ya wananchi wote wa Tandahimba.
Programu imelenga kuongeza idadi ya wateja na kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji.

# Mbarali: Mradi wa Mkunywa sasa kwa force account – Mhandisi Maryprisca




Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) amekagua utekelezaji wa mradi wa maji wa Mkunywa katika kata ya Madibira Wilayani Mbarali wenye thamani ya shilingi milioni 847 na kuelekeza utekelezaji wake umaliziwe kwa utaratibu wa force account.

Mhe. Mahundi amebaini Mkandarasi kushindwa kufanya kazi katika mradi huo pamoja na kuongezewa muda wa mkataba.
Kufuatia hali hiyo, amemuagiza meneja wa mkoa wa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) kusimamia taratibu zote za kimkataba ili kazi hiyo ambayo Mkandarasi ameshindwa ifanyike kwa kutumia utaratibu wa force account.

Mbunge mteule wa Jimbo la Mbarali Mhe. Bahati Ndingo ameishukru Serikali kwa utekelezaji wa miradi ya maji katika jimbo la Mbarali na kusisitiza kuwa Mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji wa Mkunywa amesababisha wananchi wa vijiji vya Ikoga, Mkunywa, Chalisuka, Mahango na Iheha kukosa huduma ya maji kwa wakati kwa sababu ya uzembe.
Mradi wa maji wa Mkunywa ulianza mwezi Septemba, 2022 na ulitarajiwa uwe umekamilika kwa mujibu wa mkataba mwezi Machi, 2023.








Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameshiriki katika hafla fupi ya zoezi la utiajia Saini ya Mikataba ya utekelezaji wa miradi ya Maji katika Kata ya Lepurko Wilayani Monduli mkoani Arusha.

Thamani yake ikiwa zaidi ya shilingi bilioni 27 na inatarajiwa kuhudumia zaidi ya vijiji 13 na kunufaisha wananchi zaidi ya elfu 76.
Hafla imeshudiwa na wananchi katika kijiji cha Nanja mkoani Arusha.

# Maji Tanzania Kimataifa zaidi, yaongoza



Siri na Mafanikio ya PforR Tanzania yawekwa hadharani na Aweso

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesema siri ya mafanikio katika utekelezaji wa Programu ya Lipa kwa Matokeo (PforR) ni utashi wa kisiasa na azma ya mkuu wa nchi katika kuondosha adha ya maji kwa wananchi waishio vijijini na hasa wanawake na watoto wa kike.
Amesema hayo akitoa ushuhuda wa dhamira ya Mhe Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika lengo la kumtua 'Mwanamama ndoo ya maji kichwani'.

Mhe. Aweso amesema hayo katika Mkutano wa Mawaziri wa Maji na Fedha wa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika kuhusu huduma ya maji na usafi wa mazingira Jijini Addis Ababa, Ethiopia.
Ameeleza mafanikio yametokana na usimamizi thabiti na ufuatiliaji wa karibu wa hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi, ufanyaji kazi kwa bidii na kujituma miongoni mwa watendaji wa Sekta ya Maji, utoaji wa motisha kwa watendaji wanaofanya vizuri, uwazi na matumizi sahihi ya fedha na suala zima la ujenzi wa miradi bora yenye uendelevu.

Programu ya PforR inalenga utekelezaji wa miradi ya maji vijijini. Kwa mujibu wa Benki ya Dunia Tanzania ni kinara wa utekelezaji wa Program ya PforR kati ya nchi zaidi ya 50 zinazotekeleza program hiyo huu unaoratibiwa na Benki ya Dunia.
Kufuatia maombi ya nchi mbalimbali kuhusu kujifunza nchini Tanzania utekelezaji wa Programu ya PforR Mhe. Aweso amezikaribisha kuja Tanzania.



# Sekta binafsi inamchango mkubwa katika maendeleo ya Sekta ya Maji- KM Prof. Katundu




Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu amesema serikali inatambua mchango mkubwa wa sekta binafsi katika kukuza maendeleo ya Sekta ya Maji hivyo itaendelea kupitia sera na taratibu mbalimbali ili kuhakikisha mazingira ya ushirikiano yanaendelea kuimarika.

Prof. Katundu amesema hayo wakati wa kongamano la wadau wa Sekta ya Maji la Mwaka 2023 jijini Mbeya.

Amesema serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya maji ikilenga kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma ya maji na kwamba mafanikio yote yaliyofikiwa katika lengo hilo ni makubwa na yote yamefanikiwa kutokana na ushirikiano mzuri wa Serikali na sekta binafsi.

“Nichukue nafasi hii kuwahakikishia sekta binafsi kuwa serikali inatambua mchango wenu na inaendelea kuchambua mahitaji yenu na iko tayari kushirikiana nanyi na hata kuwasaidia pale ambapo mtakakuwa mnahitaji msaada” Professa Katundu amesema.

Amewataka wadau hao wa Sekta ya Maji kujadiliana katika kongamano hilo ili kupata muongozo na utaratibu mzuri wa kuratibu shughuli za wadau wa maji ili kuimarisha ushirikiano.

Aidha, amewaagiza watendaji wa Wizara ya Maji kuwasilisha rasimu ya Sera inayoendelea kufanyiwa maboresho kwenye uongozi wa Jumuiya ya Wasambazaji wa Maji nchini (ATAWAS) ili watoe maoni na mchango wao katika kuiboresha.

Kongamano la wadau wa sekta ya maji linafanyika kwa siku tatu jijini Mbeya na limeandaliwa na Jumuia ya wasambazaji wa maji nchini (ATAWAS) likiwa na kaulimbiu isemayo “PPP for Sustainable Water and Sanitation Services ”.





*Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) na Waziri wa Fedha Mhe Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb) wakiwa katika mkutano wa viongozi wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika unaohusu masuala ya upatikanaji wa majisafi na salama na usafi wa mazingira.*

*Mkutano huu ni hatua muhimu kwa nchi za Afrika kufikia malengo ya Maendeleo endelevu ifikapo mwaka 2030.*

*Mkutano umeandaliwa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ya nchini Ethiopia, Jijini Addis Ababa.*

# Sekta binafsi yatakiwa kutumia fursa kuwekeza katika Sekta ya Maji



Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) ameitaka Sekta Binafsi kutumia fursa ya milango ya uwekezaji iliyofunguliwa na serikali ya awamu ya sita kuwekeza katika Sekta ya Maji. Wito huo ameutoa jijini Mbeya wakati akifungua kongamano la maji la mwaka 2023 lililoandaliwa na Jumuiya ya wasambazaji wa maji nchini (ATAWAS).

Amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan inatambua umuhimu wa Sekta Binafsi katika kuongeza kasi ya maendeleo kwa wananchi hivyo imekuwa ikiweka mikakati mbalimbali kuhakikisha kunakuwepo na ustawi wa sekta hiyo.

Njia hizo ni pamoja na utekelezaji wa mpango kazi wa miaka mitano kuanzia 2018 - 2023 wa namna ya kushirikisha sekta binafsi ambao umesaidia kuboresha Dawati la Ubia ngazi ya Wizara ambalo majukumu yake ni pamoja na kuratibu miradi ya ubia kati ya sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Amewashukuru wadau wote wa Sekta ya Maji kwa kusaidia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya serikali ambapo hadi sasa vijiji 9670 kati 12318 vilivyoko nchini Tanzania vimefikiwa na huduma ya majisafi na kufanya kiwango cha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kufikia asilimia 77 wakati mijini huduma ikiwa imefikia asilimia 88.

Awali akizungumza kabla ya ufunguzi wa kongamano hilo Mwenyekiti wa Bodi ya ATAWAS Mhandisi Geofrey Hill amesema mkutano huo unafanyika kila mwaka ukilenga kuwakutanisha wadau mbalimbali wa sekta ya maji ili kupata suluhisho la upatikanaji wa majisafi na salama kwa watanzania. Ameshukuru ushirikiano mkubwa wanaoupata kutoka serikalini.

Kongamano la maji la mwaka 2023 limeandaliwa likiwa na kauli mbiu isemayo “PPP for Sustainable Water and Sanitation Services” na limehudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwemo Wakurugenzi Watendaji wa Mamlaka za Maji nchini, Wakurugenzi wa Mashirika na Makampuni binafsi na Washirika wa Maendeleo.

# Chalinze washukuru kwa huduma toshelevu ya majisafi

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora na Mbunge wa Chalinze Mhe. Ridhiwani Kikwete ameishukuru serikali na Wizara ya Maji kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es salaam (DAWASA) kwa kutatua tatizo la huduma ya maji katika halmashauri ya Chalinze.

Akiongea katika kikao na Kamati ya Bunge ya Mitaji kwa Umma, amewashukuru pia wajumbe wa kamati kwa niaba ya Bunge kwa jinsi walivyosimamia kuhakikisha tatizo hilo linakwisha kwa kupitisha bajeti ya Wizara ya Maji.

Pamoja na hayo, ameishukuru DAWASA na Kaimu Mtendaji Mkuu Kiula Kingu, kwa kutenga fedha za kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Samia Suluhu Hassan alipofanya ziara jimboni hapo mwaka 2022. Katika ziara hiyo Rais Samia alielekeza kutengwa kwa shilingi milioni tano kwa ajili ya kusambaza maji katika mji wa Chalinze na viunga vyake.

Kufuatia agizo hilo, DAWASA ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 1.3 kwa ajili ya usambazaji wa huduma ya maji katika halmashauri ya Chalinze ikiwa ni mara mbili ya maelekezo yaliyotolewa na Mhe. Rais Samia.

# Aweso - DAWASA unganisheni maji kwa mfumo wa mkopo



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuhakikisha kila mwananchi anawezeshwa kupata huduma ya majisafi kwa kupewa utaratibu wa kulipa kidogo kidogo kwa mkopo.

Amesema hayo katika hafla ya utiaji saini na kumkabidhi mkandarasi M/S SINOHYDRO kutoka China eneo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji.

Amesema sio wananchi wote wanakuwa na uwezo wa kulipia gharama ya maunganisho mapya kwa wakati kulingana na utofauti wa kipato, hivyo kwa wale ambao hawawezi wapewe utaratibu wa kulipa kwa njia ya mkopo ili wote wanufaike na huduma ya majisafi.

"Kwa sasa upatikanaji wa maji kwenye maeneo mengi ya huduma umeimarika, hivyo ni vyema kila mwananchi apate huduma kikamilifu ili kufanikisha azma ya Serikali ya kumtua Mama ndoo yam aji kichwani," Mhe Aweso amesema.

"Tunapaswa kumshukuru Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa alioufanya wa fedha za ukamilishwaji wa miradi hii na usambazaji wa majisafi kwa wananchi kwenye maeneo mengi, hivyo tunapaswa kuhakikisha wananchi wanaona tija ya uwekezaji huu kwa wao kupata maji," Mhe. Aweso ameainisha.

Kuhusu mradi wa maji wa Dar es Salaam ya Kusini, amesema ni mradi mkubwa ambao utanufaisha wakazi wapatao 450,000 wa majimbo mbalimbali ya Ukonga, Segerea, Ubungo, Kibamba, Ilala na Temeke ambapo ni mradi muhimu sana kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo wamekuwa kwenye changamoto ya maji kwa muda mrefu, hivyo mkandarasi wa mradi ahakikishe anatekeleza mradi huu ndani ya wakati ili ukamilike na wananchi wapate maji.

Mbunge wa Jimbo la Segerea Mhe. Bona Kamoli ameishukuru Serikali ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuwekeza nguvu nyingi katika kumtua 'Mama ndoo ya maji kichwani' kupitia mradi huo wa maji, hivyo inaleta matumaini makubwa kwa wananchi ambao wamekuwa kwenye changamoto ya maji kwa muda mrefu.

Kwa upande wake Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA Ndugu Kiula Kingu amesema kuwa utekelezaji wa mradi huo wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji Dar es Salaam ya Kusini
Unafanikishwa kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia kwa kiasi cha shilingi bilioni 36.967.

Amesema utekelezaji wa mradi umegawanyika katika awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza utanufaisha Kata za Kwembe, Kitunda, Pugu Stesheni, Kipunguni na Mzinga. Awamu ya pili itahudumia wakazi wa Kata kata za Kivule, Kinyerezi, Zingiziwa, Majohe, Charambe, Kwembe, Buza, Msongola, Msigani na Mbezi.



# Waziri wa Maji awahakikishia wananchi wa Hanang' huduma ya maji kwa kuchukua hatua za dharura

Waziri wa Maji Mhe.  Jumaa Aweso (Mb) amesema kufuatia maporomoko na mavuriko kutoka mlima Hanang',  Wizara ya Maji inachukua hatua ya dharura kwa kuweka matanki ya maji ya dharura 30 katika kambi, vituo vya huduma za afya na maeneo yote ya vijiji vilivyoathirika katika kata za Gendahabi, Jorodom, Ganana, Katesh, Mogitu na Dumbeta.



Waziri Aweso akiwa mji wa Katesh amekabidhi kwa madiwani matanki ya maji 30 yenye uwezo wa kubeba lita 5,000 na kusema pamoja na matanki hayo, yatapelekwa magari ya kubeba maji (Maboza) matano yatakayofanya kazi ya kubeba maji kupeleka katika matenki na kufikisha huduma ya majisafi kwa wananchi.

Pamoja na hilo, amekagua mitambo ya kuchimba kisima cha maji ambayo tayari imeanza kazi ili kusaidia kuongeza maji katika vyanzo ambavyo havijaaribiwa na mafuriko. Pia, katika kurejesha huduma ya maji amekabidhi kwa wananchi bomba zenye urefu wa mita 2880.

Miongoni mwa madhara ya mafuriko hayo ni  vifo na majeruhi, uharibifu wa mali, na kuharibika kwa miundombinu ya huduma ya maji.





# Benki ya Dunia yatoa heko kwa Tanzania kuhusu Miradi ya Maji ya Lipa kwa Matokeo

Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika Dkt. Victoria Kwakwa ameipongeza Tanzania kwa kutekeleza kwa ubora na viwango Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (PforR) na kuwa kinara wa nchi nyingine Duniani zaidi ya 50 zinazotekeleza programu hiyo.

Dkt. Kwakwa ametoa pongezi hiyo jijini Addis Ababa katika mkutano wa viongozi wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika unaohusu masuala ya upatikanaji wa majisafi na salama na usafi wa mazingira.

Ameitaka Tanzania kutoa uzoefu wa mafanikio yake kwa nchi zaidi ya 23 za Mashariki na Kusini mwa Afrika zinazoshiriki mkutano huo.

Programu hiyo inatekelezwa kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia ambapo Tanzania ilipata Dola za Marekani milioni 350 katika miaka mitano na katika miaka mitatu ya kwanza ya utekelezaji ilikuwa imefikisha huduma ya maji kwa zaidi ya watu millioni 4.7 vijijini katika mikoa 17.

Kufuatia mafanikio hayo, na kulingana na matokeo , Benki ya Dunia iliongeza Dola za Marekani milioni 300 na hivyo kuongeza wigo wa utekelezaji na kufikia mikoa 25, hivi sasa shillingi milioni 970 zimepelekwa katika kila Halmashauri nchini Tanzania ili kuanza utekelezaji.

Mafanikio ya PforR yamefungua milango ya uendelevu wa programu hiyo ambayo itafikia ukomo Julai 2025. Hivyo, Kufuatia hoja ya Tanzania ya kuwa na PforR Awamu ya Pili, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kuwa na PforR Awamu ya Pili katika kipindi cha 2025-2030.

Programu ya PforR imewezesha Wizara ya Maji kufanikisha miradi ya maji 1,500 ambayo inatoa huduma kwa maefu ya wananchi.







*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri ameitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kuhakikisha miradi ya maji inayotekelezwa inaonekana kwa thamani ya fedha.*

*Maelekezo hayo ametoa katika kikao cha ufuatiliaji wa maendeleo ya mradi wenye thamani ya shilingi bilioni 185 na kusisitiza kuwa utekelezaji wa mradi huo upo nyuma ya muda na ipo haja ya kuongeza kasi*

*Amewataka Wataalam Washauri wa Mradi huo kukamilisha nyaraka za zabuni ifikapo Disemba 2023.*

*Amewasisitiza kufanya kazi kwa ushirikiano na kushirikisha wadau ili kuleta tija na matukio mazuri katika utekelezaji wa mradi huo.*

# Mwaka mpya 2024 kuwa neema ya kuwafaidisha majisafi zaidi ya wananchi elfu 75.9 wa Nzuguni



Wananchi na wakazi wa maeneo ya Nzuguni,Kisasa,Ilazo,Mwangaza, Mwanyika na Swaswa katika Jiji la Dodoma wataondokana na adha ya uhaba wa huduma ya majisafi mapema Januari Mosi, 2024 kufuatia utekelezaji wa ujenzi wa mradi mkubwa wa maji wa Nzuguni wenye thamani ya shilingi bilioni 4.3 utekelezaji wake kufika asilimia 96.
Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule akifanya kazi ya ufuatiliaji wa mradi huo amewahakikishia wananchi wa Mkoa wa Dodoma kuwa changamoto ya uhaba majisafi itaondoshwa ifikapo mwezi Januari, 2024 mradi utakapokamilika, na hilo ndio matumaini makubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuwaondolea wananchi wake adha ya uhaba wa huduma adhimu ya majisafi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Dodoma (DUWASA) Mhandisi Aron Joseph ambaye ndiye mtekelezaji na msimamizi wa mradi huo amesema ujenzi wa mradi ulianza tarehe 07 Februari , 2023 na utakapokamilika na kuwanufaisha zaidi ya wananchi elfu 75.9 na kufanya ongezeko la asilimia 11 ya hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kutoka wastani wa asilimia 50 hadi asilimia 61.7 kwa siku.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Dodoma,Mhe. Alhaj Jabir Shekimweri aliyeambatana na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dodoma katika ziara hiyo ya ukaguzi wa maendeleo ya ujenzi wa mradi wa maji -Nzuguni amempongeza Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), pamoja timu yake yote kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maji mkoani Dodoma, na kwamba kukamilika kwa mradi wa majisafi Nzuguni kutasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza adha ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi, pia ameipongeza DUWASA kwa kuanza awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa maji kwa kuanza kuchimba visima vitano vya maji.

# Tuwe wazalendo na miradi yetu - Mhe. Majaliwa




Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) amezitaka Taasisi na Mashirika ya Umma kote nchini yanayotekeleza miradi mbalimbali kuwa na uzalendo na kuweka mbele maslahi ya taifa.

Mhe. Waziri Mkuu Majaliwa amesema hayo ikiwa ni matokeo ya kutekelezwa kwa weledi,ufanisi, kiwango na uzalendo mkubwa kwa Mradi wa Maji wa Itumba-Isongole wilayani Ileje,mkoa wa Songwe,akiweka jiwe la msingi la mradi huo.

Mhe. Waziri Mkuu amempongeza Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso ((Mb na Naibu wake , Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb) pamoja na wataalamu wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa usimamizi mzuri wa fedha za mradi wa maji wa Itumba -Isongole na kutekeleza mradi huo kwa gharama ya shilingi bilioni 2.6 kati ya bilioni 4.9 ambazo zilitengwa ili kutekeleza mradi huo,hivyo kubaki kwa fedha ya serikali ambayo itatekeleza miradi mingine ya maji, na kwamba ni vema watekelezaji wa miradi ya serikali wakajenga utamaduni wa uzalendo na uadilifu katika matumizi ya fedha za umma.

Naibu Waziri wa Maji, Mhe. Mhandisi Mary Prisca Mahundi (Mb) amemuwakilisha Waziri wa Maji, katika ziara hiyo iliyifanywa mkoani Songwe na Waziri Mkuu mwishoni mwa mwezi Novemba 2023.

Mhe. Godfrey Kasekenya, Mbunge wa Jimbo la Ileje ameipongeza Wizara ya Maji kwa utekelezaji wa mradi wa maji wa Itumba-Isongole ambao utaondoa kabisa tatizo la hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa asilimia 100 wilayani Ileje na kuwa na ziada ya maji.

Mradi wa Maji wa Itumba-Isongole katika Wilaya ya Ileje,mkoani Songwe unatekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Taifa wa Maji ( NWF) na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Disemba 2023 na utahudumia wananchi zaidi ya elfu ishirini wa miji ya Itumba na Isongole wilayani Ileje.

# Zimbabwe waja kujifunza kuhusu huduma ya maji Tanzania





*Timu ya watalaamu kutoka Serikali ya Zimbabwe wakiwa nchini kwa siku tatu kujifunza kuhusu mabadiliko makubwa katika utoaji wa huduma ya maji kwa wananchi. Wataalamu hao ni watumishi wa kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nchini Zimbabwe.*

*Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Prof. Jamal Katundu akiwa pamoja na watendaji wa taasisi za Wizara ya Maji katika kazi ya kuandaa Mpango Mkakati na kutumia mfumo wa kieletroniki wa kufanikisha majukumu pamoja na kupima utendaji kazi wa watumishi katika wizara. Lengo ni kujenga umiliki na kuwa pamoja katika kufanikisha malengo ya Serikali katika Sekta ya Maji kuhakikisha huduma bora kwa wananchi*







# Taarifa ya hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa kuzingatia idadi ya watu kwa mwaka 2025 dhidi ya malengo ya kufikia asilimia 95 mjini Bunda.





1.0 UTANGULIZI.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda hutoa majisafi kwa wakazi wa Bunda mjini na viunga vyake, hii inajumuisha mitaa ya Nyabehu, Guta, Tairo,Nyantare na Migungani ambayo bomba kuu linaloleta maji Bunda mjini limepita.Chanzo cha maji kinachotumika ni cha uhakika(Ziwa) ambalo lina maji ya kutosha kwa ajili ya kuwahudumia Wananchi wa Mjini Bunda.Hadi sasa Mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira Bunda ina jumla ya Km za 427.15 mtandao wa bomba wenye vipenyo mbali mbali na Matangi ya maji yenye ujazo wa lita 2,265,000 na maji hutolewa kwa wasitani wa masaa 22 kwa siku.

2.0 HALI YA UPATIKANAJI WA HUDUMA YA MAJI (WATER SERVICE COVERAGE REPORT) KWA KUZINGATIA IDADI YA WATU YA MWAKA 2025 THIDI YA MALENGO YA KUFIKIA ASILIMIA 95 MIJINI.

Halmashauri ya mji wa Bunda ina jumla ya kata (14) ndani ya mji wa Bunda ambavyo inakadiriwa kuwa hadi sasa Bunda Mjini una wakazi 182,970 (2022) kutokana na sensa ya mwaka 2022.Na kwa sasa inakadiriwa kuwa eneo linalo hudumiwa na Mamlaka ya majisafi na Usafi wa Mazingira Bunda una wakazi 191,936 (2023) kati ya hao asilimia 77.01% ndiyo wanaopata huduma kwa sasa ambayo ni sawa na wakazi 147,818 kufikia mwezi August 2023.

3.0. HALI YA UZALISHAJI MAJI.

Mamlaka ya majisafi na usafi wa Mazingira Bunda ina uwezo wa kuzalisha maji kutoka kwenye chanzo kipya Nyabehu lita za ujazo 10,800,000/ kwa siku ambacho kimekamilika mwaka 2023 na pia kupitia chanzo cha maji cha zamani lita za ujazo 4,464,000 na kufanya jumla ya lita za ujazo 15,264,000

Kati ya jumla ya lita za ujazo 14,784,000 Mamlaka ina uwezo wa kuzalisha lita 5,160,000 kwa siku kutokana na ufinyu wa mtandao wa bomba kutofikia Wananchi wote Mjini Bunda,hivyo Mamlaka ina akiba ya maji ya kutosha ya lita za ujazo 9,624,000 ambazo zinaweza kufikia service coverage ya 95 kufikia Mwaka 2025 endapo tutaongeza mtandao wa bomba kufikia maeneo yote na kupanua bomba za kusafirisha maji tokea Migungani hadi kwenye tangi za mlima bombani ili pampu mbili ziweze kufanya kazi kwa wakati mmoja na kubadili bomba la GRP linalopeleka maji tokea kituo cha Kusuma maji Mingungani hadi tangi liliyoko mlima Boman na kuweka bomba za chuma ili kuzuia upotevu mkubwa wa maji unaotokea kwa sasa.

# BILIONI 1.6 NDANI YA MWAKA MMOJA YAIPENDEZESHA TABORA.

UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ina wakazi wapatao 308,741 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022. Mahitaji ya maji kwa mji wa Tabora kwa sasa ni mita za ujazo 29,438 kwa siku ambapo asilimia 94 ya wakazi wa Tabora wanapata huduma ya majisafi, vyanzo vya uzalishaji wa maji vina uwezo wa kuzalisha jumla ya mita za ujazo 57,842 kwa siku.

Hali ya upatikanaji wa majisafi ni matokeo ya kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kwa kutekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka ziwa Viktoria mkoani Mwanza kupitia miji ya Shinyanga, Igunga, Nzega, Isikizya hadi manispaa ya Tabora. Zaidi ya shilingi bilioni 640 zimetumika kufanikisha mradi huo mkubwa ambao ulikamilika mwezi Februari mwaka 2020.

Ni wazi kuwa ongezeko la uzalishaji wa majisafi baada ya matumizi ni ongezeko la majitaka kwa sababu wataalamu wa masuala ya maji wanasema asilimia 80 ya majisafi yanayotumika hugeuka na kuwa majitaka. Hivyo, uzalishaji wa majitaka kwa manispaa ya Tabora kwa sasa unakadiriwa kufikia lita 15,600,000 kwa siku.

Mjini Tabora yapo maeneo ambayo yamekuwa na changamoto kuhusu maji machafu, hususan kata zilizopo bondeni za Ng'ambo, Gongoni, Kitete, Tambukareli, Malolo, Isevya, Ipuli pamoja na Cheyo. Maeneo haya wakati wa mvua mifumo ya vyoo imekuwa tabu kwa kujaa na kulazimika kuvuta maji machafu mara kwa mara.

Maji hayo yalikuwa yakimwagwa katika mabwawa yasiyokuwa na kiwango stahili yalipo maeneo ya Milambo Barracks. Mabwawa hayo yalijengwa ili yatumike kwa muda mfupi na kwa sasa hayana uwezo wa kutibu majitaka kufikia kiwango kinachoruhusiwa kumwagwa kwenye mazingira au kutumika kwa kilimo kutokana na ongezeko kubwa la uzalishaji wa majitaka.





MTANDAO WA MAJITAKA

Mji wa Tabora umeunganishwa na mtandao wa majitaka katika kata za Gongoni, Kanyenye na Kiloleni wenye urefu wa km. 23 pamoja na malambo makubwa matatu (3). Sehemu kubwa ya mfereji wa majitaka imepita kwenye maeneo ya Taasisi za Umma hivyo mtandao uliopo unatumika chini ya uwezo wake kwasababu Jiografia ya maeneo yenye wakazi wengi bado haijaruhusu kutiririsha majitaka katika mfereji huo.

CHANGAMOTO

I. Mtandao wa majitaka katika Manispaa ya Tabora upo katika sehemu ndogo tu ya katikati ya mji ambapo ni asilimia 8.4 ya wakazi ndio wameungwa katika huduma hii. Asilimia 91.6 wanatumia vyoo vya shimo pamoja na septic tanks. Vyoo hivi vya mashimo vimekuwa havikidhi mahitaji ya watumiaji hususani wakati wa mvua.

II. Maeneo ya Kata zilizopo bondeni za Ng'ambo, Gongoni, Kitete, Tambukareli, Malolo, Isevya, Ipuli pamoja na Cheyo, vyoo vimekuwa vikijaa maji wakati wa majira ya mvua na hivyo kulazimika kunyonya mara kwa mara kwa kutumia magari ya majitaka na kwenda kumwaga kwenye mabwawa yasiyo na ubora yaliyopo Milambo Barracks.

III. Mabwawa hayo yalijengwa ili yatumike kwa muda mfupi na kwa sasa hayana uwezo wa kutibu majitaka kufikia kiwango kinachoruhusiwa kumwagwa kwenye mazingira au kutumika kwa kilimo kutokana na ongezeko kubwa la uzalishaji wa Majitaka.

MAJIBU YA KUPUNGUZA CHANGAMOTO

Serikali kwa kuona umuhimu wa Usafi wa Mazingira kupitia Wizara ya Maji imetoa kibali kwa TUWASA kujenga mabwawa mapya makubwa ya kutibu Majitaka yanayokusanywa kwa njia ya magari kutoka kwenye makazi na sehemu za biashara eneo la Mirambo barracks kwa lengo la kuboresha mazingira ya manispaa pamoja na afya za wananchi.

UTEKELEZAJI WA MRADI

Utekelezaji wa mradi huu unagharimu kiasi cha shilingi Billioni moja, Millioni mia sita ishirini na nane, Mia nane thelathini elfu, mia mbili themanini na tisa na senti sabini na sita tu (1,628,830,289.76).

Mradi unatekelezwa na Mkandarasi kampuni ya Peritus Exim Private ya Dar Es Salaam. Ujenzi wa mradi ulianza rasmi tarehe 29 Machi, 2023 na unatarajiwa kutekelezwa kwa miezi kumi na mbili (12). Pia, kazi zifuatazo zitafanyika;-

(i) Ujenzi wa mabwawa mawili (2) aina ya Anaerobic yatakayotumika kupokelea majitaka yanayoletwa na magari.

(ii) Ujenzi wa mabwawa mawili aina ya Facultative yanayotumika kutibu majitaka kibailojia.

(iii) Ujenzi wa ardhi oevu (wetland) kwa ajili ya kusafisha maji zaidi na kuondoa vimelea,nutrients.

(iv) Ujenzi wa chemba mbili (2) za kumwagia majitaka kutoka katika magari/maboza .

(v) Ujenzi wa eneo la kukaushia taka ngumu (Drying beds) .

(vi) Ujenzi wa nyumba ndogo maalum kwa ajili ya kuchomea taka ngumu (Incinerator)

(vii) Ujenzi wa uzio kuzunguka mabwawa.

(viii) Ununuzi wa gari moja (1) la kubeba majitaka.

MATARAJIO BAADA YA KUKAMILIKA MRADI

Mradi huu utakapokamilika, utaboresha usafi wa mazingira na afya kwa wananchi wa manispaa ya Tabora, utatoa fursa ya kilimo cha mbogamboga kwa kuwa maji yatakayotoka yatakidhi viwango vinavyotakiwa kwa kilimo cha umwagiliaji. Pia, mradi utaongeza ajira hasa katika hatua ya ujenzi na kipindi cha uendeshaji wake.

Bodi na Menejimenti ya TUWASA inatoa shukrani kwa Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na viongozi wa Wizara ya Maji kwa kujali afya za Watanzania wote wakiwemo wakazi wa Manispaa ya Tabora.


WIZARA YA MAJI
KHERI YA SIKUKUU YA
Noeli na
Mwaka Mpya
2024
"Tulinde na Tutunze miradi
na vyanzo vya maji "
ww.maji.go.tz



**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz